**25-Faharasa**

| Neno | Maana Yake |
|---|---|
| 'Aaridhw as-Sukuwn | sukuwn pana ya kusimami neno. |
| 'Ibaadah | ibada |
| Ahkaamut-Tajwiyd | Hukumu za Tawjiyd |
| Alfaadhw | Matamshi. Tamshi moja ni 'lafdhw' |
| Arjah | Iliyo na nguvu kabisa, inayodhaniwa kuwa sahihi kabisa, rai inayokubalika kabisa. |
| Ar-Rawm | Maana ya asil ni ombi.<br><br>Katika Tajwiyd ni kuifanya vokali au irabu kuwa dhaifu hadi kwamba ipotee sauti yake, au kutumia sehemu ya vokali au irabu. Hivyo ni kutamka kwa haraka vokali au irabu katika neno la mwisho analosimamia msomaji huku ikisikika. |
| As-Sakt | Kipumziko bila ya kushusha pumzi |
| Azaaimu sujuwd | Sijda zilizoazimiwa au zilizoruhusiwa; Sijda zilizosisistizwa katika kusoma Qur-aan |
| Basmalah | BismiLLaah - kwa Jina la Allaah |
| Dhikri , dhikru-Allaah | Kumdhukuru Allaah kwa kila aina; kukumbuka Utukufu Wake, neema Zake, ihsani Yake kwa kutaja jina Lake; kumsabbih, kumpwekesha, kumshukuru, kumsifu, kumtukuza, kuomba maghfirah, kusoma Qu-raan, kumswalia Mtume (صلى الله عليه وسلم), na kwa kuzingatia na kuyataamali Majina Yake Matukufu. |
| Dhwamiyr | Kiwakilishi nomino |

| | |
|---|---|
| Dhwammah | Vokali au irabu ya ‘u’ |
| Dhwammatayn, | Vokali mbili za ‘u’ |
| Faqiyh | Mwanachuoni aliyebobea katika somo la fiqhi. |
| Fardh ‘ayn | Wajib wa kila Muislamu kutekeleza jambo fulani la sheria ya Kiislamu. |
| Fardhi kifaayah | Wapatikane baadhi ya watu kutenda jambo fulani la sheria ya Kiislamu hivyo huwa imetosheleza katika jamii ya Kiislamu. |
| Fat-haa | Vokali au irabu ya ‘a’ |
| Fathatayni | Vokali au irabu mbili za ‘a’ |
| Ghunnah | Sauti inayotoka puani ya mvuto wa harakah mbili |
| Hamzatul-Qatw’ | Hamzah ya kukata |
| Hamzatul-Waswl | Hamzah ya kuunga |
| Harakah/Harakaat | Kipimo cha mvuto wa madd kukadiria urefu wa sauti (kwa hesabu ya sekunde) |
| Herufi za hawaaiyyah | Herufi za hewa |
| Herufi za Hijaaiyyah | Herufi za alfabeti |
| Hukmu | Hukumu, kanuni |
| I’raab | Irabu au vokali; fat-hah, kasrah, dhwammah, sukuwn, na tanwiyn |
| Idghaam | Kuunganisha au mlishizo wa herufi kwa herufi nyingine. |
| Ikhtilaas | Maana ya asili ni kunyakua vokali au irabu kwa haraka hata ibakie vokali au irabu kidogo. Katika riwaaya ya Hafs ‘an ‘Aaswim ikhtilaas |

| | |
|---|---|
| | inatekelezwa katika neno moja tu nalo ni katika Suwrat Yuwsuf (12:11)<br><br>تَأۡمَنَّا |
| Imaam<br>Maimaam | Imamu- kiongozi wa Dini kama vile katika kusalisha.<br><br>Maimamu – ujumla wa imamu |
| Ish-maam | Maana yake ya asili ni kuchanganya. Katika Tajwiyd ni kuchanganya herufi au vokali. Na katika riwaayah ya Hafsw 'an Aaswim maana pekee ni kuufanya mdomo uchanganye kutamka vokali au irabu ya dhwammah (u) pamoja na sukuwn. |
| Isti'aadhah | Kuomba kinga kutokana na shaytwaan kwa kusema 'Awdhu BiLLahahi minash-Shaytwaanir-rajiym |
| Jannah | Pepo |
| Jarr | Vokali au irabu ya 'i' |
| Jawwada | Ni kufanya jambo vizuri. Katika Tajwiyd ni kuisoma Qur-aan ipasavyo kwa hukmu za Tajwiyd. Anaposema mtu "Jawwadal-Qur-aan" maana yake ameisoma Qur-aan kwa uzuri kabisa kama ipasavyo kwa hukmu za Tajwiyd. |
| Kasraa | Vokali au irabu ya 'i' |
| Kasratayni | Vokali au irabu mbili za 'i' |
| Lafdhw Al-Jalaalah | Kutamka jina la ﷲ Allaah (سبحانه وتعالى) |

| | |
|---|---|
| Lahn | Maana ya asili ni kutamaka kimakosa. Katika Tajwiyd ni kukosa kuisoma Qur-aan kwa hukmu za Tajwiyd ambako kunapelekea kufanya makosa ya dhahiri au ya kufichika. |
| Lahnul-Jaliy | Makosa ya dhahiri (Makubwa) |
| Lahnul-Khafiy | Makosa ya kufichika (Madogo) |
| Madd | Mvuto wa herufi |
| Maddiyah | Za madd |
| Maddul-Aswlliy | Madd ya asili, asilia |
| Maddul-Far'iy | Madd ya matawi |
| Maddut-Twabiy'iy | Madda ya asili, asilia. |
| Maf-'uwl / Maf-'uwlun-bih | Katika nahw ya lugha ya Kiarabu inayomaanisha: kitu au mtu aliyetendewa kitendo. |
| Makhaarij Al-Huruwf/ | Matokeo ya herufi |
| Makhraj | Sehemu moja ya kutokea herufi |
| Makruwh | Inachukiza |
| Mandhwumah | Maana ya asili; mfumo, njia, utaratibu fulani. Maana ya ki-shariy'ah ni shairi au qaswiydah linaloundwa kufanya mukhtasari wa funzo la somo fulani. |
| Mujtahid | Mtu anayefanya jihaad katika mambo ya Dini, kama kutafuta elimu, kufundisha, kufanya da'awah n.k |
| Munaasib | |
| Mushaddad | Iliyo na shaddah |
| Mutabaa'id | Zinazowekana/zinazokuwa mbali |
| Mutajaanis | Zinazoshabihiana |

| | |
|---|---|
| Mutakhasw-swiswuwn | Watu walioshughulika zaidi na jambo fulani; mfano waliobobea katika somo la Tajwiyd. |
| Mutamaathil | Zinazaofanana sare |
| Mutaqaarib | Zinazokaribiana |
| Mutawaatir | Mapokezi yaliyopokewa na watu wengi (vipindi mbali mbali vya miaka) kutoka kwa watu wengi mfano wao, na inakuwa si rahisi kwao wao kupokea riwaayah za uongo. |
| Nabrah kugongeka | Kugongeka kwa herufi. Kupanda sauti ya herufi inapotamkwa. |
| Naswb | Vokali au irabu ya 'a' |
| Nuskhah | kopi |
| Nutqw | tamko |
| Qaadhwi | Kadhi |
| Qaariu/Qurraa-ah/ Maqurraa-ah | Msomaji/Wasomaji/Wasomaji |
| Qamariyyah | Herufi zinazojulikana kuwa ni herufi za mwezi; ni zile ambazo hazikuingiwa na shaddah baada ya alif na lLaam na hivyo kuifanya laam itamkwe. |
| Qiblah | Kibla |
| Qiraa-ah , qiraat | Kisomo |
| Quraysh | Kabila la Waarabu waliokuwa Makkah kabla ya Uislamu na baada yake. |
| Raawiy | Mpokezi wa Hadiyth au kauli |
| Raf-'u | Vokali au irabu ya 'u' |

| | |
|---|---|
| Rakhaawatihaa | Udhaifu au ulaini wake |
| Riwaayah | Upokezi |
| Riyaa-a | Riya – kujionyesha katika ibada au jambo la kheri linalomshirikisha Allaah (سبحانه وتعالى) kama ni shirki ndogo. |
| Sajdatu-Tilaawah | Sajda ya kisomo |
| Salafus-Swaalih' | Waja wema waliotangulia |
| Shamsiyyah | Herufi zinazojulikana kwa ni herufi za jua; ni zile ambazo zenye kuingiwa na shaddah baada ya alif na laam na hivyo kuifanya laam isitamkwe. |
| Shariy'ah | Sheria, hukmu ya Dini ya Kiislamu. |
| Shaytwaan | shetani |
| Sijjdah sajdah, sujuwd | sijda |
| Sunnah muakkadah | Sunnah iliyosisitizwa |
| Swifaat Al-Huruwf | Sifa za herufi |
| Swiffah | Sifa |
| Taabi' Taabi'iyn. | Aliyefuata waliofuata. Kizazi cha tatu baada ya karne ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) . Ali |
| Tafkhiym | Kutamka kwa kuifanya herufi nzito kwa kujaza mdomo |
| Takkbiyrah | Kumtukuza Allaah (سبحانه وتعالى) kwa kusema "Allaahu Akbar" |

| | |
|---|---|
| Talaqqiy | Kusoma Qaariu mbele ya mwanafunzi uso kwa uso kisha mwanafunzi anamfuatiliza qiraa-ah chake. |
| Tarqiyq | Kutamka kwa kuifanya herufi iwe hafifu bila ya mdomo. |
| Tartiyl | Kusoma Qur-aan kwa utaratibu upasao. |
| Tilaawah | Usomaji (Qur-aan) |
| Twahaarah | Tohara – kuwa katika hali ya kukuruhusu kutekeleza ‘amali kadhaa za ‘ibaadah. Pia ni kufanya udhu, ghuslu. |
| Twariyq Ash-Shaatwibiyyah | Twariyq ni njia.<br><br>Ash-Shaatwibiyyah ni jina la Imaam Ash-Shaatwibiyy.<br><br>Shaatwibiyyah ni jina la shairi liloandikwa na Imaam Ash-Shaatwibiyy kuhusu viraa saba, likajulikana kwa umaarufu “Qaswiydah Ash-Shaatwibiyyah fil-qiraatis-sab-‘”. Twariyq (njia) hii ya Ash-Shaatwibiyyah ndio njia maarufu ambayo aghlabu ya Waislamu wanaisoma Qur-aan. |
| Twariyq Twayyibatin-Nashr | Hukmu alizoziandika Imaam ibn Al-Jazariyy kuhusu Viraa kumi katika kitabu chake: “An-Nashr fil Qiraatil-‘ashr”. Shairi aloandika kuwepesisha kujfunza njia hizo linaitwa “Twayyibatun-Nashr fil-qiraat al-‘ashr” Na njia hizo zinaitwa “Twariyq Atw-Twayyibah”. |
| Ummah | Umati/umma |
| | |

| | |
|---|---|
| | |
| | |
| | |